

Somo La 4

BIBLIA: KUCHAGUA TOLEO LA KIINGEREZA

Somo la pili na la tatu lilitupa maelezo ya jumla kuhusu Biblia ilivyopitishwa hadi kufikia uchapishaji wa Toleo Jipya na uvumbuzi wa Vitabu vya Bahari ya Chumvi. Ni miswada na matoleo ya watu wakuu tu ndiyo yametajwa. Kwa hakika, kuna matoleo zaidi ya 700 na nyingine tele ambayo yamewahi kuwepo. Tangu karne hii ipite, matoleo kadhaa ya Kiingereza na tafsiri za Biblia zimetufikia. Kujaribu kununua Biblia siku hizi ni balaa tupu kwa mwanafunzi makini wa Biblia anayetaka ile iliyo sahihi. Swali kuu ni tafsiri au toleo lipi ndilo bora zaidi? Ni ipi inayowakilisha kikweli neno asili la Mungu?

Kwanza, twafaa kutambua kwa masikitiko ya kuwa hakuna toleo lililo kamili la Kiingereza. Lugha iliyotumiwa mwanzo kuandikia Biblia si Kiingereza. Biblia “kamili” ingefaa ile ambayo mswada wake asili umetumia lugha asili – Kiebrania (Agano la kale) au Kiyunani (Agano Jipya). Biblia tulizonazo kwa leo ziko mbali sana, ingawa, kama tulivyokwisha kuona, uhifadhi wake umekuwa wa hali ya juu.

JINSI YA KUTATHMINI MATOLEO YA BIBLIA

Kuna jinsi tatu ya kutumia ili kufikia uamuzi wa akili pevu na uchaguzi ulioangaziwa vema.

- Namna ya tafsiri
- Imani ya mtafsiri – hasa kuhusiana msukumo
- Ukiangalia nakala iliyotumiwa katika utafsiri

Katika somo hili tutachunguza vigezo hivi kimoja baada ya kingine ili uweze kuvitumia katika kufanya uamuzi unapochagua toleo la Biblia.

1. AINA YA TAFSIRI

Biblia za Kiingereza na pia za Kiswahili hutafsiriwa kulingana na njia mojawapo kati ya hizi nne:

1. Mbinu ya mtindo wa ulinganifu rasmi
2. Mbinu ya usawa wa elimumwendo
3. Mbinu ya ufafanuzi
4. Mbinu ya tafsiri ya maridhiano

Kila mojawapo ya mbinu hizi zina tabia tofauti ambazo twafaa kuzifahamu kabla ya kuchagua toleo la Biblia.

a) Sifa bainifu ya mbinu ya mtindo wa ulinganifu

Tafsiri ya neno kwa neno (kwa usahihi kama lugha ya mapokezi itakavyoruhusu hali hiyo) inakaribia sintaksi ya lugha ya asili – tafsiri isiyo na mapendeleo – aina bora kwa wasomi makini wa Biblia; ikiwa mtu anataka kufahamu ujumbe uliofunuliwa hasa wa maandiko – pia ni vizuri kwa mambo yanayohusu ibada kwa kuwa inafuatilia kwa karibu lugha asili.

Mifano ya matoleo ya Biblia Inayotegemea Sifa Bainifu ya Ulinganifu Rasmi

- King James Version
- Revised Version
- American Standard Version
- Revised Standard Version
- New American Study Bible
- New King James Version
- New Revised Standard Version

b) Sifa za Mbinu ya Usawa Wa ElimuMwendo

Tafsiri inayoangalia maana kwa maana (maana ya nakala aili inatafsiriwa katika hali ambayo mtafsiri anaona ni sawa na wazo la lugha ya mapokezi) na humpa mtafsiri nafasi ya kuweza kuhamisha athari yake katika nakala iliyotafsiriwa na mambo mengi wazo la kuvuviwa kwa pumzi ya Mungu, mafundisho, istilahi, na maneno yapotea hivyo na huu ndio mtindo unaotumiwa sana na vyama vya Biblia katika kazi nyingi za utafsiri ambao sio wa Kiingereza.

Mifano ya matoleo ya Biblia Inayoegemea Mtindo huu wa usawa wa Elimu-Mwendo

- Good New Bible(pia yajulikana leo hii kama English Version)
- New English Bible

c) Sifa Za Mbinu Ya Ufafanuzi

Sio tafsiri ya kweli, mfafanuzi anaweka kitu tofauti katika maneno na hatumii lugha asili kama msingi bali anafanua kutoka kwa kazi ya tafsiri.

- Haufuati mfumo wa utaratibu maalum, hatua kwa hatua, kwa hivyo inategemea fikira na imani ya mfafanuzi.
- Ni nukuu, sio neno la Mungu bali ni jinsi mtu anavyofikiri au matakwa yake huyo
- Kwa mfano, Yohana 1: 1-2 (Living Bible) “Kabla ya kuwepo kitu chochote, Kristo alikuwepo pamoja na Mungu. Amekuwa hai tangu hapo na yeye mwenyewe ni Mungu.”

Hii ni nukuu potovu ukiangalia msembo asili wa kifungu hiki. (Linganisha na KJV, RSV, NKJV)

Mifano Ya Matoleo Ya Biblia Zinazofuata Mtindo wa Ufafanuzi

- New Testament in Modern Speech
- Living Bible
- d) **Sifa Za Mbinu Ya Tafsiri Ya Maridhiano**
- Maridhiano kati ya mtindo wa ulinganifu rasmi na mtindo wa usawa wa elimu-mwendo
- Ni vigumu sana mwanafunzi wa Biblia kutambua wakati fasili ni halisi na wakati ambao sio.
- Kwa mfano, Wafilipi 2:8 – (NIV) “Ambaye, asili yake hasa ni Mungu...” – ni ufafanuzi; “... hakudhania kuchukua hali sawa na Mungu...”
- Ni tafsiri ya moja kwa moja (yaani, mtindo usio na msimamo)

Mfano wa matoleo ya Biblia inayotegemea mbinu ya tafsiri ya maridhiano

- New International Version
- New Jerusalem Bible
- Revised English Bible

2. IMANI YA MTAFSIRI

Kitu kingine kinachoweza kuathiri usahihi wa toleo ni imani ya wale wanaotafsiri kufuatia fundisho la uvuvio wa Roho Takatifu.. Ikiwa watafsiri hawaamini kabisa kuwa Biblia nzima ni kazi ya pumzi ya Mungu, patakuwa na kipenye cha kuongozwa na “uhakiki wa juu” (higher criticism) – inayoweza kuleta matokeo ya sehemu Fulani ya Biblia kuachwa nje. Panaweza tokea mielekeo katika utafsiri ya kudhoofisha kanuni ya uvuvio/wahyi (pumzi ya Mungu), au mwelekeo wa kuingiza maneno ya uongo yanayohitilafiana na sehemu zingine za Biblia.

Wanaotafsiri pia wanaweza kuwa na upendeleo wa kibinafsi.

Katika matoleo mengine, kumekuwepo na mwelekeo wa ulegevu wa msimamo huria; yaani, kueleza maandiko kwa dhana na kanuni katika hali ya mawazo huru yasiyo ili kuwapendeza wengi au kuwa na msimama wa siasa inayokubalika kuliko ilivyostahili kwa lugha pokezi.

Mwelekeo wa hivi punde ni ule wa tafsiri za kisasa zinazoitwa jinsia jumuishi (inclusive gender), ambayo kwa kweli hubadilisha jinsia asili ili kujumuisha wanawake ambapo kwa lugha ya mapokezi ilionyesha wazi ni waume (kwa mfano, 1 Timotheo 3:2, 1 Timotheo 3:12 NRSV) Katika lugha ya mapokezi hapana ruhusa ya kufanya hivyo.

3. NAKALA YA KIMSINGI

Chaguo Lililopendekezwa (Kuanzia Juu Katika Orodha Inayopendelewa)

1. King James au New King James Version (Kwa utafiti makini)
2. New American Standard Bible
3. Revised Standard Version
4. Revised Version
5. New American Standard Bible

Mapendekezo na mashauri mengine

Tafuta Biblia iliyo na nafasi pembezoni kuandika vitu vya kukumbusha au tanbihi chini ya ukurasa ikitoa maelezo zaidi ikiwezekana. Biblia yenye nafasi pana pembeni yafaa sana ikiwa utapenda kujiandikia makala ya kumbukumbu ya kibinafsi.

Toleo la King James Version laendelea kutumika kwa utafiti makini kwa sababu takribani vitabu vingi vya marejeleo ya maandiko kama vile Strongs' Concordance, Englishman's Hebrew na Greek Concordance, Thayer's Lexicon, Vine's Expository Dictionary, nk.vinaegemea msingi wa nakala ya King James Version.

New King James Version hasa ni King James Version katika Kiingereza cha sasa, ikiwa na marekebisho ya makosa ya uandishi yaliyosahihishwa, kwa sababu ya mabadiliko haya, ni vigumu wakati mwingine kutumia vitabu vya marejeleo na kazi zingine za utafiti kutegemea msingi wa nakala za kitambo za KJV.

Vitabu vingine vya marejeleo na za utafiti vimefanyiwa marekebisho mapya ili vipate kwenda sambamba na NKJV. Jaribu kuvipata ikiwa wapendelea toleo la NKJV.

New International Version yaonyesha ishara ya kuwa toleo linalopendwa na wengi kuliko King James Version. Ingawa ni kama bahati mbaya mambo kuwa hivi, lakini si jambo la kutamausha; cha msingi ni kuwa, msomi makini ataangalia upungufu wa NIV na apate kuelewa na kuwekea alama sehemu au vifungu tatanishi. Na pia, machapisho ya hivi punde ya kamusi sanifu na vitabu vya utafitii vinavyotumika sambamba na NIV vitasaidia pakubwa.

Kuongezea kwa Biblia Yenye msingi wa Ulinganifu Rasmi (k.m King James Version), ni jambo bora kuwa na matoleo ambayo sio ya tafsiri ya moja kwa moja ili kufanya ulinganifu, na sio utafiti makini. Badala yake mtu anaweza kupata toleo mbadala wenye maelezo pembezoni.

Usitegemee sana “Biblia tafiti” isipokuwa kwa kufanyia marejeleo tu. “Utafiti” huo umefanywa na mapadri weledi na inaelekea upande wa mawazo ya kidini yaliyokubalika. Ni utafiti uliotiwa koponi, na katika hali waweza kumvunja moyo Yule anayefanya utafiti wa kibinafsi.

Kama ilivyo kawaida kwa mtu kulinganisha andiko moja na lingine ili kujua maana ya kifungu, ni vema pia kulinganisha matoleo mbalimbali ili kufikia uamuzi bora wa Biblia mwafaka ya kutufaa kwa haja yetu.

Utafiti zaidi juu ya jambo hili umependekezewa wale wanaotaka mwelekeo huo. Utafiti huu umerahisishwa na kazi nyingi na maandishi ya wanazuoni na watu wenye uwezo mkubwa; na mwanafunzi atafaidika kwa kupata elimu inayofaa kwa kutumia vitabu vinavyohusu maandiko ambavyo vipi.

Kufupisha yote yaliyojadiliwa juu ya jambo hili, yavutia kuona nukuu ya mkurugenzi wa awali wa makavazi ya Uingereza inayojumuisha mengi ya miswada ya Kale akisema:

“Mkristo anaweza kuchukua Biblia nzima mikononi mwake na aseme bila uoga au kusita kuwa ameshikilia neno la kweli la Mungu, ambalo limepokezwa pasi na kitu kupotea kutoka kizazi hadi kizazi katika karne zote.”

Maswali ya somo la 4

1. Ni kigezo kipi kati ya tatu za mwanzo kinachotumiwa katika kuchagua Toleo la Biblia?
2. Ni kigezo gani cha pili kati ya tatu kinachotumiwa katika uchaguzi wa toleo la Biblia?
3. Ni kigezo kipi cha tatu ambacho lazima kutumika katika kuchagua Toleo La Biblia?
4. Orodhesha mbinu au mitindo minne ya kutafsiri Biblia.
5. Ni mtindo upi una matokeo bora ya Toleo La Biblia, inayofaa kwa utafiti makini wa Biblia?
6. Ni mtindo upi usiofaa sana? Kwa nini?
7. Imani ya wale watafsiri kuhusu pumzi ya Mungu, uvuviaji wa Roho Takatifu unawezaje kuathiri matokeo ya Utafsiri?
8. Ni nini twaweza kuangalia kama sifa ya kimsingi ya nakala ya toleo lolote lile?
9. Matokeo yapi ndiyo “Chaguo lililopendekezwa” katika somo hili?
10. Ikiwa itatokea hali ambapo uchaguzi utalenga New International Version, mtu atakuwa na matarajio yapi?
11. Kwa nini ni vema mtafiti makini wa Biblia asitegemee sana “Biblia Tafiti”?